

KUMB: PPR/14 - 6/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATANO, TAREHE 4 Juni 2014**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 4 Juni 2014**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo.

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 7 Mei 2014. Katika toleo hili, bei ya rejareja kwa Petroli na Mafuta ya Taa imeongezeka kwa Sh 10/lita sawa na asilimia 0.44% na Sh 19/lita sawa na asilimia 0.9% sawia, ambapo bei ya rejareja ya dizeli imeshuka kwa Sh 16/lita, sawa na asilimia -0.73%. Kwa kulinganisha matoleo haya mawili, bei ya jumla kwa mafuta ya Petroli na Mafuta ya Taa pia zimeongezeka kama ifuatavyo Sh 9.67/lita sawa na asilimia 0.46% ,Sh 18.82/lita sawa na asilimia 0.98% sawia, na Dizeli imeshuka kwa Sh 15.55/lita sawa na asilimia -0.76%. Mabadiliko haya yametokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani.
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap) kama ilivyokokotolewa na fomula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 432 la tarehe 29 Novemba 2013.**
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
Dar es Salaam	2,210	2,125	2,046
Arusha	2,294	2,209	2,130
Arumeru (Usa West)	2,294	2,209	2,130
Karatu	2,313	2,227	2,148
Monduli	2,300	2,214	2,135
Ngorongoro (Loliondo)	2,351	2,265	2,186
Kibaha	2,215	2,129	2,051
Bagamoyo	2,221	2,136	2,057
Kisarawe	2,218	2,132	2,053
Mkuranga	2,220	2,135	2,056
Rufiji	2,238	2,152	2,074
Dodoma	2,269	2,184	2,105
Bahi	2,276	2,191	2,112
Chemba	2,295	2,210	2,131
Kondoa	2,302	2,216	2,137
Kongwa	2,266	2,181	2,102
Mpwapwa	2,270	2,185	2,106
Iringa	2,274	2,189	2,110
Kilolo	2,279	2,193	2,114
Mufindi (Mafinga)	2,284	2,199	2,120
Njombe	2,302	2,217	2,138
Ludewa	2,340	2,255	2,176
Makete	2,333	2,248	2,169
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,300	2,215	2,136
Bukoba	2,425	2,340	2,261
Biharamulo	2,400	2,314	2,235
Karagwe (Kayanga)	2,442	2,356	2,277
Kyerwa (Ruberwa)	2,447	2,362	2,283
Muleba	2,425	2,340	2,261
Ngara	2,391	2,305	2,226
Misenyi	2,434	2,348	2,269
Geita	2,375	2,290	2,211
Bukombe	2,364	2,279	2,200
Chato	2,396	2,311	2,232
Mbogwe	2,413	2,328	2,249

Nyang'hwale	2,390	2,305	2,226
Kigoma	2,441	2,356	2,277
Uvinza (Lugufu)	2,453	2,368	2,289
Buhigwe	2,430	2,345	2,266
Kakonko	2,398	2,313	2,234
Kasulu	2,427	2,342	2,263
Kibondo	2,406	2,320	2,241
Moshi	2,284	2,198	2,120
Hai (Bomang'ombe)	2,287	2,202	2,123
Mwanga	2,277	2,192	2,113
Rombo (Mkuu)	2,305	2,219	2,141
Same	2,270	2,185	2,106
Siha (Sanya Juu)	2,291	2,205	2,126
Lindi	2,269	2,184	2,105
Kilwa Masoko	2,244	2,159	2,080
Liwale	2,290	2,205	2,126
Nachingwea	2,298	2,213	2,134
Ruangwa	2,296	2,211	2,132
Babati	2,333	2,247	2,168
Hanang (Katesh)	2,343	2,258	2,179
Kiteto (Kibaya)	2,344	2,258	2,179
Mbulu	2,345	2,260	2,181
Simanjiro (Orkasumet)	2,364	2,279	2,200
Musoma	2,389	2,303	2,224
Rorya (Ingirijuu)	2,397	2,312	2,233
Bunda	2,380	2,294	2,215
Butiama	2,385	2,300	2,221
Serengeti (Mugumu)	2,434	2,349	2,270
Tarime	2,400	2,314	2,235
Mbeya	2,317	2,232	2,153
Chunya	2,327	2,241	2,162
Ileje	2,330	2,245	2,166
Kyela	2,333	2,247	2,169
Mbarali (Rujewa)	2,301	2,216	2,137
Mbozi (Vwawa)	2,327	2,241	2,162
Momba (Chitete)	2,335	2,250	2,171
Rungwe (Tukuyu)	2,326	2,241	2,162
Morogoro	2,235	2,150	2,071
Mikumi	2,251	2,165	2,087
Kilombero (Ifakara)	2,273	2,188	2,109
Ulanga (Mahenge)	2,284	2,198	2,119

Kilosa	2,254	2,168	2,089
Mvomero (Wami Sokoine)	2,246	2,160	2,081
Turian	2,260	2,175	2,096
Mtwara	2,283	2,197	2,118
Nanyumbu (Mangaka)	2,331	2,246	2,167
Masaki	2,308	2,223	2,144
Newala	2,315	2,229	2,150
Tandahimba	2,308	2,222	2,143
Mwanza	2,360	2,275	2,196
Kwimba	2,396	2,311	2,232
Magu	2,368	2,283	2,204
Misungwi	2,366	2,280	2,201
Sengerema	2,393	2,307	2,228
Ukerewe	2,420	2,334	2,255
Sumbawanga	2,383	2,297	2,219
Kalambo (Matai)	2,375	2,290	2,211
Nkasi (Namanyelee)	2,396	2,311	2,232
Katavi (Mpanda)	2,418	2,332	2,253
Mlele (Inyonga)	2,396	2,311	2,232
Songea	2,334	2,248	2,169
Mbinga	2,367	2,282	2,203
Namtumbo	2,363	2,277	2,198
Nyasa (Mbamba Bay)	2,369	2,284	2,205
Tunduru	2,392	2,307	2,228
Shinyanga	2,339	2,253	2,175
Kahama	2,353	2,267	2,188
Kishapu	2,367	2,282	2,203
Simiyu (Bariadi)	2,380	2,295	2,216
Busega (Nyashimo)	2,373	2,288	2,209
Itilima (Lagangabilili)	2,383	2,298	2,219
Maswa	2,372	2,286	2,207
Meatu (Mwanhuzi)	2,379	2,293	2,214
Singida	2,301	2,215	2,137
Iramba	2,313	2,227	2,149
Manyoni	2,285	2,200	2,121
Ikungi	2,296	2,211	2,132
Mkalama (Nduguti)	2,325	2,240	2,161
Tabora	2,364	2,279	2,200
Igunga	2,318	2,233	2,154
Kaliua	2,382	2,297	2,218
Ulyankulu	2,376	2,291	2,212

Nzega	2,329	2,243	2,164
Sikonge	2,376	2,291	2,212
Urambo	2,377	2,292	2,213
Tanga	2,256	2,171	2,092
Handeni	2,236	2,150	2,072
Kilindi	2,270	2,185	2,106
Korogwe	2,249	2,164	2,085
Lushoto	2,259	2,174	2,095
Mkinga (Maramba)	2,271	2,185	2,106
Muheza	2,256	2,171	2,092
Pangani	2,263	2,178	2,099

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	2,108.42	2,022.90	1,944.03

Miriam Mahanyu
KNY:MKURUGENZI MKUU
EWURA

